Badiliko La Moyo

(Changes Of The Heart)

Na

Ellis P. Forsman

Badiliko La Moyo
(Changes Of The Heart)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Badiliko La Moyo

Zaburi 19:1-14

Zaburi 19:14, "*Maneno ya kinywa change, na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee BWANA, mwamba wangu na mwokozi wangu.*"

Neno "*moyo*" imetumika mara nyingi katika biblia.

1 Pet. 3:1-4, "*Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu kusudi ikiwa wako wasioliamini neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile neno; wakiutazama mwenendo wenu safi, na wa hofu. Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani kusuka nywele na kujitia dhahabu na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani roho ya upole na utulivu, iliyo na thamani kuu mbele za Mungu.*"

Tafsiri ya Vine: "Moyo unatumiwa kwa uhalisia kwa ajili ya mtiririko wa maisha binafssi yaliyojificha."

Moyo unajumuisha "*utu uliojificha*", au utu wa ndani ambao Petro aliandika. Ni sehemu ya mwanadamu iliyotayari kupenda, kuchukia, furaha, imani, nk. Kwanzia kuzaliwa hadi mbinguni, kila mmoja anapita mabadiliko ya moyo wa ndani.

Kwa wakati huu tutaangalia baadhi ya mabadiliko haya.

Moyo Mweupe (Umezaliwa hauna hatia)

Weupe unahusishwa na usafi na utakaso. Biblia inaitumia kuelezea kana kwamba mtu hana dhambi.

Watoto wadogo hawarithi dhambi binafsi. Lakini hurithi kifo binafsi.

- Rum. 5:12, "*Kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi;*"
- Ebr. 9:27, "*Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja na baada ya kufa hukumu;*"
- Marko 10:14, "*Ila Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao.*"
- Mat. 18:3, "*Akasema, Amin, nawaambia, msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.*"

Mkimbiza farasi mzuri magharibi mwa “B” kiujumla walionwa wamevaa kofia nyeupe na wanaendesha farasi mweupe. Mwendelezo, watu wabaya walivaa kofia nyeusi na kuendesha farasi weusi.

Michael Medved, muandaaji wa sinema za taifa alisema sinema ya leo inaonyesha mashujaa waakifanya mambo mabaya. Haishangazi kwamba thamani ya ulimwengu huu umedidimia.

Roho Nyeusi (imejaa dhambi)

Kwa umri wa kuhesaabiwa, roho inatenda dhambi. Roho inakuwa mdanganyifu. Yer. 17:9, “*Moyo huw mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?*”

Historia ya Biblia inafunua dhambi ya mwanadamu.

- Mwanzo 6:5, “*BWANA akaona ya kuwa maovu ya wanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote.*”
- Rum. 1:24-25, “*Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao, waufuate uchafu hata wakavunjiana heshima miili yao. Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina.*”
- Rum. 3:9, “*Ni nini basi? Tu bora kuliko wengine? La! Hata kidogo. Kwa maana tumekwisha kuwashitaki Wayahudi na Wayunani ya kwamba pia wamekuwa chini ya dhambi;*”
- Rum. 3:23, “*Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*”
- 1 Yoh. 1:8-10, “*Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu.*”

Roho Ya Hudhurungi (toba)

Mungu anakubali roho inayohuzunika kwamba imetenda dhambi (huzuni na kujutia, huzunika). Zaburi 51: 17, “*Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu hutaudharau.*”

Kabla ya toba ni lazima mtu awe na imani.

Kura ya hivi karibuni ilionyesha kwamba %14 ya Wamarekani wanaamini kwamba Biblia hakika ni neno la Mungu; wengi wanaamini ndiyo lakini maoni ya waandishi wa kale.

- 1 Thes. 2:13, "*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokeaa si kama neno la wanadamu bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendaalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.*"

- 2 Kor. 7:10, "*Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti.*"

Toba ni badiliko la nia liletalo badiliko la tendo.

Moja ya tatizo lililopo katika mazungumzo ya Ukristo ni kwamba watu hawataki kubali baadhi ya matendo yao. Badiliko haalikufanywa katika mioyo yao.

Mifano miwili ya huzuni: Watu wawili wanaongelea juu ya kahawa. Kufikia sukari, mmoja wao kwa bahati mbaya anagonga kikombe chake cha kahawa upande mwingine. Hatua halisi la tendo hilo linapaswa liwe, "Mimi ni mpumbavu kiasi gani. Ningejua vyema. Angalia uchafu huo nilioufanya. Samahani." Huzuni inayojenga ni tofauti. Mwenye hatia anapaswa kusema, "Samahani. Kunakitambaa hapa. Nitafuta meza." Pia anapaswa kumlipa mfuta meza. Huzuni ya kimungu inajenga, pamoja na huzuni.

Tukiwa katika hali ya dhambi, ni sawa na kuendesha baiskeli kwenye upepo – Mungu anaonekana kuwa kinyume nasi. Vile vile, ni kama mwendesha baiskeli akikatisha na kuona kwamba upepo unamsaidia, tutakuta kwamba Mungu anafanya kazi pamoja nasi kama tukitubu na kubadilisha mwelekeo wa maisha yetu. Mungu hakubadilika – bali **sisi**.

"Mifano isiyo ya kibiblia".

- Petro anatuambiaa kuwa Nuhu alikuwa "*mhubiri wa haki*" (2 Pet. 2:5), lakini ujumbe wake kabla hajaingia ndani ya safina haikuwa, "Kitu kizu kinakwenda kukutokea!"

- Amosi hakukabiliwa na kuhani mkuu wa Israeli kwa kutangaza, "Kukiri ni kumiliki!" Yeye, kama nabii wa Mungu, aliionya Israeli kwamba wataadhibiwa kwa kukosa kwao.

- Yeremia hakuwekwa kwenye tundu kwa kuhubiri, Nipo SAHIHI.; uko SAHIHI." Mungu, akinena kupitia Yeremia, aliiambia Israeli itubie uovu wao na hata waangamiza.

- Yohana Mbatizaji hakukatwa kichwa chake kwa sababu alihubiri, "Tabasamu, Mungu anakupenda!" Alihubiri toba alipokuwa katika nyika, na alipomuonya Herode kwamba haikuwa sheria kwake kwamba aishi na mke wa nduguye.

Ujumbe ulikuwa ni upi wa watu hawa wa Mungu? Neno moja: "Tubu!"

Moyo Mwekundu (imefunikwa na damu ya Kristo)

Mtu anapotenda dhambi, na akazitubia dhambi zake kweli, bado anahitaji msamaha wa dhambi hizo.

Hii inawezekana kupitia damu ya Yesu.

- Efe. 1:7, "*Katika yeye huyo kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*"
- Ebr. 13:12, "*Kwa ajili hii Yesu naye ili awatakase watu kwa damu yake mwenyewe, aliteswa nje ya lango.*"
- Rum. 8:1, "*Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.*"

Mtu anaingiaje ndani ya Kristo?

- Rum. 6:4, "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"
- Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmevaa Kristo.*"
- Isa. 1:18, "*Haya njooni tusemezane, asema BWANA. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.*"
- Ebr. 9:22, "*…na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.*"
- Mdo. 2:38, "*…Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

Moyo Mweupe (msamaha)

Mara mtu akibatizwa, anakuwa kiumbe kipya katika Kristo.

- 2 Kor. 5:17, "*Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya.*"
- Tito 3:3-6, "*Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukizana.*"
- Efe. 4:22-24, "*Mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho na nia zenu; mkavae utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.*"
- 1 Yoh. 1:7-9, "*Bali tukienenda nuruni kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo ndani mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote.*"

Moyo Wa Waridi (moyo wenye furaha)

Wakristo wanapaswa kuwa watu wenye furaha katika dunia.

Towashi wa Kushi. Mdo. 8:26-39, "*Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza nayo ni jangwa. Naye akaondoka akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu; akawa akirejeaameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo, sogea karibu na gari hili ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, je yamekuelea hayo unayosoma? Akasema, nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjioni kama kondoo, na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule towashi*

akamjibu Filipo akasema, nakuomba, nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake, naye akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji, yule towashi akasema tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akasema naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi."

Nafurahi kwa sababu dhambi zake zimesamehewa na ana taraja la maisha ya milele mbinguni.

Wakristo mara nyingi watakuwa na mateso hapa, lakini kama tukiwa kama mitume, bado tu tutakuwa na furaha.

- Mdo. 5:41, "*Nao wakatoka katika lile baraza wakifurahi kwa kuwa wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya jina hilo.*"
- Mdo. 16:25, "*Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza.*"
- Fil. 4:4, "*Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema furahini.*"

Moyo Wa Kijani (ukuaji)

Moyo ni lazima ukuwe la sivyo itakufa kiroho.

- 1 Pet.2:2, "*Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.*"
- 2 Pet. 3:18, "*Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokovu Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*"

Mazoezi ya kiroho ni muhimu. 1 Tim. 4:7-8, "*Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini uzikatae; nawe ujizoeze kupata utauwa. Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwa faa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani unayo ahadi ya uzima wa sasa, nay a ule utakaokuwapo baadaye.*"

Madaktari wanadai kwamba tukiufuata mfumo wa mazoezi kila wakati, tutapata majibu yanayofaa ya uzito kupungua na uimara wa

mwili. Tukiujaribu, hatupati matokeo ya papo kwa hapo. Katika majuma machache ya kwanza tunakuwa wadhaifu, uchovu, na maumivu. Siri ni kuvumilia. Kwa muda mrefu, mazoezi huleta mafanikio mazuri ya hali ya mwili. Mfumo huo huo unaendana na utii. Kila mara haiko vizuri, lakini kwa muda mrefu, inaleta matokeo mazuri.

Ramani Ya Kweli (uaminifu)

Hii ni muhimu, kwa waaminifu pekee watakaoingia mbinguni.

- Ufu. 2:10, "*Usiogope mambo yatakayokupata; tazama huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa , nami nitakupa taji ya uzima.*"
- 1 Kor. 15:58, "*Basi ndugu zangu wapendwa, mwimarike msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana.*"

Tabia zetu ni zipi kuhusu uaminifu? Je tunajali uaminifu wetu kama tunavyoujali katika nyanja zingine za maisha?

- Kama magari yetu huwaka mara moja kwa kila mara tatu, inakubalika?
- Kama kijana anayekuuzia magazeti akishindwa kukupitishia kila Jumatatu, je atakuwa mwaminifu?
- Kama friji yako ikiacha kufanya kazi kwa siku moja au mbili kila wakati, je utasema, "Oh, sawa, inafanya kazi mara nyingi?
- Kama kile kifaa cha umeme kinachochemsha maji kinaleta maji ya baridi wakati wa kuoga kila wakati, utasema inategemea?
- Kama ukikosa malipo ya mikopo kila mwaka, je benki itasema, "Kumi ya kumi na mbili siyo mbaya?
- Kama ukishindwa kumwabudu Mungu kama Bibilia inavyoelekeza, je utatarajia kuitwa Mkristo mwaminifu?

Tunatarajiaa uaminifu na uwepo katika vitu na watu wengine. Je Mungu hatarajii hivyo kutoka kwetu? Tunajiona wenyewe kama waliojitolea katika maisha yetu ya kidini kuliko majukumu yetu yanavyotufunga? Kwa aliyejitolea, karibia kila kitu kinaonekana kukubalika. Kwa mtumwa aliye katika kifungo cha zamu, uaminifu unatarajiwa kwake.

Mat. 25:21, "*Bwana wake akamwambia vema, mtumwa mwema na mwaminifu, ulikuwa mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.*"

Moyo Wa Dhahabu (mbinguni)

Mbingu imeandaliwa maalum kwa wale waliojiandaa wenyewe.

Yohana 14:1-4, "*Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo. Nami niendako mwaijua njia.*"

Hii inapaswa kuwa ndoto ya kila Mkristo.

Kufika mbinguni, kila mtu anapaswa kuwa na roho yake imeandaliwa katika uzima wa milele.

Hitimisho

Je una shida ya moyo? Hali ya moyo wako ukoje? "Roho yako iko sawa na Mungu?"

Mtu anapataje roho safi? Lazima afanyike Mkristo.

Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6, "*Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana yeye ajye kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ndiye, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17) kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na ya kwangu aliniambia kuwa aamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nikachukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamab kuna Mungu. Lakini ilikuwa sehemu yenye usalama, niheri aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) katika siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu atamuruhusu aingie mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

  Matend 11:18, *"...Mungu amewajalia hata mataifa nao toba iletayo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, ukafikiria mwenyewe, "*kuna mwizi humu ndani!*" Na unachukua simu yako na kuwa pigia polisi, ukiwambia kuwa kuna mwizi nyumbani kwako. Muda mfupi unasikia wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi lazima aombe msaha kwamba hataiba tena na kubadilisha maisha yake. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kufanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba kifungu hicho kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba tayari amesha pata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa. Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akambatiza. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*" (Math. 3:14-17).

  Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "imekuwa kwetu **sisi** "*kuitimiza haki yote*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

  Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, umesema ni nini maana ya

ubatizo? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi.*" Kwa nini yeyote anaweza kuacha hatua inayotuondoa dhambi?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tuzikwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Paulo (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile "*Sasa unakaawilia nini? Simama, na ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.*" (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Waru 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani yake Mungu kwa kupaka damu yake Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kaburini kwa kuweka udongo mdogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?